CAMBRIDGE
International Education

# Cambridge IGCSE™

**SWAHILI** **0262/02**

Paper 2 Listening **May/June 2025**

TRANSCRIPT **Approximately 45 minutes**

This document has **8** pages. Any blank pages are indicated.

© Cambridge University Press & Assessment 2025



https://xtremepape.rs/

**Eng:** Cambridge Assessment International Education
Cambridge IGCSE® Examination in Swahili
Paper 2 Listening, May/June 2025
Turn over now.

*(Pause 5 seconds.)*

**TLR: Zoezi 1**

Utasikia vipande vinane vifupi vilivyorekodiwa.
Jibu swali 1–8 katika nafasi uliyopewa.
Majibu yako yawe mafupi iwezekanavyo.
Utasikia kila rekodi mara mbili.

**TLR:** Swali 1

**M:** * Rukia, hebu nikumbushe, wewe ni Mkenya au Mtanzania?

**F:** Mama yangu ni Mkenya ingawa mimi nimezaliwa Tanzania. Tumekuwa tukija huku Kenya tangu nilipokuwa mtoto mchanga ili kuwatembelea ndugu zetu.

**M:** Alaa kumbe!

**F:** Ndio. Hata hivyo, ingawa tumehamia mwaka uliopita, nimeshazoea kuishi hapa kwani nina kumbukumbu za likizo zangu huku. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**TLR:** Swali 2

**F:** * Mazingira huku kwetu yanavutia wengi. Kuna milima na mabonde ambayo huwapa furaha, hasa watu wanaopenda kutembea masafa marefu. Mimi huhisi raha zaidi katika nchi tambarare ambapo wanyama wadogo kama sungura huishi. Ukitembea huko, lazima utawaona na kufurahi. Dada yangu anapendelea milima zaidi kwani yeye ni mtu wa mazoezi. Mwaka uliopita, alifika kilele cha Longonot ambapo aliwaona wanyama wakubwa kama twiga na punda milia. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**TLR:** Swali 3

**M:** * Hivi Wangui, ulienda kwenye maandamano ya kusherehekea ushindi wa timu yetu ya mpira?

**F:** Tofauti na Asha aliyenyimwa ruhusa ya kuenda na mama yake, mimi nilienda kwani mama hakuwa na wasiwasi wa kuwepo kwa hadhira kubwa katika maadhimisho. Ilikuwa muhimu sana kwangu kuenda.

**M:** Hata mimi! Nilifika mapema ili kumwona nahodha wetu kwenye basi la timu akibeba kikombe, lakini niliondoka umati ulipozidi. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*



https://xtremepape.rs/

**TLR:** Swali 4

**F:** * Ningependa kupata wafadhili ili niweze kukimbia mbio za mji wetu. Pesa za wafadhili zitanisaidia kununua viatu vya kukimbilia na pia nguo za mazoezi. Lakini kwanza, ninakusudia kujipiga video huku nikionyesha adhima yangu ya kukimbia. Ninahisi watakaoiona hawatakuwa na kinyongo cha kunifadhili. Kocha wangu anataka nishughulikie lishe yangu kabla ya vitu vingine vyote, lakini mimi sioni ulazima, niko tayari kabisa. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**TLR:** Swali 5

**M:** * Hivi mama yako anafanya kazi gani?

**F:** Hivi sasa yupo nyumbani anatulea tu sisi lakini alituma maombi ya kazi sehemu nyingi, na ana miadi ya kuhojiwa kwa kazi ya ualimu wiki ijayo.

**M:** Ni katika shule yako?

**F:** Hapana ni shule nyingine. Nisingependa kuwa shuleni kwangu. Kabla ya kutuzaa, alikuwa mwanasayansi na anatuhadithia kuhusu mapenzi yake kwa masomo ya kemia. Kwa bahati nzuri, shule yangu haina nafasi ya mwalimu wa kemia! **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**TLR:** Swali 6

**M:** * Huku niambia ilikuwaje ulipohamia Morogoro, unapapenda?

**F:** Ndio, ni mji wenye hali ya hewa nzuri sana. Nimepanga kuzurura mjini wiki ijayo ili nipafahamu zaidi.

**M:** Wazo zuri sana. Na vipi shule yako mpya, nzuri?

**F:** Ingawa ilikuwa kubwa mno na sikuwapenda walimu wote, nilikuwa na raha tele kuhudhuria shule yangu ya zamani kwani nilikuwa na marafiki wengi walionifahamu vizuri. Hii shule mpya si mbaya lakini sina ari ya kuenda shule ninapoamka asubuhi.

**M:** Nimekuelewa, pole. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**TLR:** Swali 7

**F:** * Nimefikia kwenye hoteli ambapo kifungua kinywa huwa tayari kuanzia saa moja asubuhi hadi saa nne, na pia chakula cha jioni kinapatikana kuanzia saa kumi na mbili jioni. Mgahawa wa chakula upo juu kabisa, kwenye ghorofa ya kumi. Lakini wakati mwingine, mimi ninapendelea kujipikia mwenyewe katika jiko dogo. Jiko lipo kwenye ghorofa ya kwanza ambalo huwa wazi kuanzia saa tatu hadi saa kumi jioni. Kwa hivyo ninaweza kula ninachokitaka. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

© Cambridge University Press & Assessment 2025 

https://xtremepape.rs/

**TLR:** Swali 8

**M:** * Unasoma lugha gani shuleni?

**F:** Katika shule yetu unaweza kusoma lugha kama Kiarabu na Kichina, ambazo nimehisi ni ngumu mno kuzisoma. Kwa hivyo nilichagua kusoma Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa.

**M:** Alaa! Na kwa nini unapendelea lugha hizo?

**F:** Kusema kweli mimi hupasi Kiingereza kwa sababu ninapenda kutazama filamu za lugha hiyo kwa hivyo ninakielewa vizuri. Lakini, kwa vile sisi husafiri sana Afrika mashariki, ninazungumza Kiswahili fasaha na ndiyo lugha inayonivutia hasa. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**TLR:** Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 1. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 2. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 2.

*(Pause 30 seconds.)*

**TLR: Zoezi 2**

Utamsikia msichana anazungumza kuhusu kundi la wanamuziki la watoto huko Uganda.
Msikilize na malizia sentensi.
Andika neno moja au maneno mawili tu katika kila nafasi.
Utasikia rekodi mara mbili.

**F:** * Hivi karibuni kundi la wachezaji muziki la watoto wadogo kutoka Uganda linaloitwa Watoto Dhahabu limevuma kote ulimwenguni. Sababu kuu ni kutendeka kwa jambo ambalo halikuwahi kutokea katika historia ya onyesho walilokuwamo. Siku hiyo kengele maalumu iligongwa katikati ya onyesho lao katika kipindi maarufu cha televisheni huko Uingereza. Baada ya kengele kulia, vikaratasi vya rangi tofauti vilidondoka kutoka kwenye paa na kutua jukwaani ambapo vilisambaa kote. Hii iliashiria ushindi, na kwamba onyesho lao ni zuri kuliko yote.

Kikundi hiki ni uthibitisho wa upendo unaoletwa na kucheza muziki. Kikundi kimekuwa mitandaoni kwa miaka kadhaa, ambapo wao hucheza nyimbo mbalimbali na kutoa video kwenye majukwaa kama YouTube, Instagram na TikTok. Video zao hutazamwa na watu milioni 25 au zaidi, na wanajulikana kwa sababu hiyo. Ungefikiri kuwa maarufu ni lengo lao kuu, lakini Watoto Dhahabu wenyewe wanahisi fahari kutokana na upekee wa sanaa yao.

Wao huchanganya mila na ubunifu na hivyo kundi hili huonekana likicheza katika kijiji cha jadi cha Kiafrika, ambapo kuna mandhari ya vijijini, ingawa watu wamevaa nguo za enzi. Wao hufuata maadili ya jadi na ushawishi wa kisanii. Kwa kutoonyesha Afrika kama sehemu iliyojaa umaskini, wanasaidia kuondoa taswira potofu inayoendeleza tatizo la ubaguzi. Pia wao hucheza kwa mbwembwe na kuonyesha furaha.

Lakini je, Watoto Dhahabu ni akina nani? Wao ni sehemu ya familia ya watoto 40 wanaolelewa katika nyumba ya yatima. Nyumba hiyo imekuwa ikitoa malazi, chakula na elimu kwa watoto kutoka mitaa ya Kampala tangu mwaka 2007. Ingawa hawakuwa na marupurupu katika maisha yao, walikuwa na umoja kati yao. Walianza kucheza muziki mwaka 2013 kufuatia mafanikio ambayo hawakuyatarajia waliyoyapata baada ya kucheza video ya dansi iliyotengenezwa nyumbani kwao. Baada ya kushinda, walipata pesa zilizowasaidia watoto hao wanaoishi katika mazingira magumu kupata maisha bora. **

*(Pause 30 seconds.)*

© Cambridge University Press & Assessment 2025 

https://xtremepape.rs/

**TLR:** Sasa sikiliza tena.

*(Pause 3 seconds. Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 2. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 3. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 3.

*(Pause 30 seconds.)*

**TLR: Zoezi 3**

Utawasikia watu sita wakizungumza kuhusu malazi chuo kikuu.
Oanisha wasemaji na mawazo katika orodha **A–G**. Kwa kila msemaji, andika herufi (**A–G**) katika mstari wa jibu.
Tumia kila herufi mara moja tu. Kuna herufi ya ziada isiyohitajika.
Utasikia rekodi mara mbili.

**TLR** * Msimulizi 1

**M:** Nilishaamua chuo nitakachokitaka tangu nilipokuwa mtoto. Dada yangu alinichukua kumtembelea rafiki yake aliyekuwa akisoma huko. Nilivutiwa na majengo mapya ambamo wanafunzi walikuwa na vyumba vyao. Kila chumba kilikuwa na choo chake, kwa hivyo wanafunzi hawakuwa na shida ya kutumia vyoo vya umma. Hata hivyo, walitumia jiko moja, na walipeana zamu kupika. Hakukuwa na ratiba ya kusafisha jiko kwani chuo chao kililipia usafi. Papo hapo nikakumbuka jinsi ninavyolazimika kusafisha chumba changu nyumbani na kuamua kwamba nitaenda chuoni hapo nitakapokuwa mkubwa.

**TLR:** Msimulizi 2

**F:** Mimi nitakuwa mtu wa kwanza kuenda chuo kikuu katika familia yangu. Kusema kweli tangu nilipokuwa mdogo nilijiuliza kama kuna umuhimu wa kuenda kusoma chuo kikuu kwani wazo la kuishi na watu wengi huku tukigombania kutumia choo na jiko halinivutii kabisa. Nina familia kubwa na nimechoka kugombania vitu. Ningalikuwa na pesa ningependa kukodi nyumba nzima ambamo ningeishi wakati wa masomo yangu. Sivutiwi na wazo la kukaa nyumbani wakati wa masomo.

**TLR:** Msimulizi 3

**M:** Niliweza kuwekeza pesa nyingi nilipokuwa nasoma chuo kikuu. Chuo chenyewe kipo mkabala na nyumbani kwetu kwa hivyo sikuhitaji kulipia nyumba nyingine. Kwa vile mimi ni mtoto pekee, nina chumba changu nyumbani kwetu hivyo sikuona sababu ya kuhama. Chumba changu kina dawati la kusomea na pia rafu la vitabu, pia mtandao mzuri sana. Bila shaka mama alinilazimisha kusafisha chumba mwenyewe na pia kusaidia kazi za nyumbani, hasa kuhusu jiko, lakini kuna starehe ya kuendelea kuwa nyumbani.

**TLR:** Msimulizi 4

**F:** Ninahisi ni lazima kuhama nyumbani wakati wa kuenda chuo kikuu na kuishi kwenye bweni au kukodi mahali ambapo utajifunza kujitegemea na kujitayarisha kwa maisha ya baadaye. Tatizo kuu nililokuwa nalo ni kuweza kupangilia pesa zangu vizuri. Sijazoea kufanya bajeti, hivyo hujichanganya kuhusu mambo ya kuwekea kipaumbele. Nitajifunza yote haya nikianza kuishi mwenyewe. Jambo ambalo nina uhakika nalo ni kwamba ninavutiwa na majengo yanayoonekana makongwe mno kwani huwa na harufu tofauti.



https://xtremepape.rs/

**TLR:** Msimulizi 5

**M:** Ni muhimu kupenda mahali unapoishi; mimi ninavutiwa na nyumba kongwe zenye historia, kama chuo changu kilichojengwa karne chache zilizopita. Tatizo pekee ni choo kwani zamani hawakujenga vyoo ndani ya chumba, hivyo wanafunzi wote wanalazimika kutumia choo kwa pamoja. Kwa vile mimi sipendi kutumia choo kilichochafuliwa, ninalazimika kuamka mapema sana ili nikoge kwa raha. Kama ningekuwa naenda chuo kikuu katika mji ambao familia yangu inaishi, nisingekubali kubaki nyumbani, ningetaka kuishi kwenye bweni la wanafunzi.

**TLR:** Msimulizi 6

**F:** Marafiki zangu ni watu ambao nimeishi nao bwenini. Mwanzoni, hatukuwa na uhakika wa kupatana kwani sote tulitoka sehemu tofauti kabisa. Baada ya miezi kadhaa tukawa marafiki wakubwa. Pia nilisafiri kimasomo muhula uliopita ili niweze kuboresha Kiswahili changu. Nilienda Lamu na huko ilibidi kukaa nyumbani kwa mwenyeji wa pale. Niliishi kwenye nyumba kongwe na ilikuwa na harufu iliyonivutia. Kabla ya safari nilikuwa na hofu kwani wenyeji wana desturi tofauti nami, lakini niliwapenda sana. **

*(Pause 5 seconds.)*

**TLR:** Sasa sikiliza tena.

*(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

**TLR:** Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 3. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 4. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 4.

*(Pause 30 seconds.)*

**TLR: Zoezi 4**

Utasikia mahojiano katika redio kuhusu kazi ya mwanaakiolojia.
Sikiliza mazungumzo hayo na soma maswali.
Kwa kila swali chagua jibu sahihi kati ya **A**, **B** au **C**.
Weka alama ya tiki kwenye kisanduku sahihi.
Utasikia rekodi mara mbili.

**F:** * Pamoja nasi leo kwenye studio ni mwanaakiolojia, yaani mwanahistoria anayechimba ardhi kutafuta vifaa vya zamani ambaye anaitwa Ahmed Juma. Tafadhali tuambie, je elimu yako ilikutayarisha kwa kazi uifanyayo sasa?

**M:** La hasha. Nilipokuwa mtoto nilikuwa na hamu ya kuwa dereva wa gari la abiria. Mimi nililelewa katika nyumba ambapo nilikuwa na uhuru wa kufanya nilichotaka na wazazi wangu walikuwa na shughuli zilizowafanya wasikae nyumbani sana. Ninadhani nilikua huku nikitamani kuwa nao na nilifikiri kuendesha gari kungenipeleka kule walipokuwapo. Niliwaona wenzangu wakisafiri na wazazi wao na kwa kweli nilitamani sana kama wazazi wangu wangekuwa nyumbani zaidi.

**F:** Alaa, na shule ilikuwaje?

**M:** Kusema kweli sikupenda shule kabisa na niliwacha shule kabla hata ya kuhitimu masomo yangu ya shule ya upili. Hadi hivi sasa hata sina cheti cha kuonyesha nilichokisoma shuleni. Ninafikiri walimu wangu pia waliniona kama mtoto mtukutu, tofauti na wengine waliopenda kuwa shuleni.

**F:** Sasa ukafanya nini baada ya kuacha shule?



https://xtremepape.rs/

**M:** Jambo la kwanza nililolifanya ni kutafuta meli ili nifanye kazi ya ubaharia. Nilipata meli na nilisafiri nchi nyingi ingawa sikupata pesa za kuweza kuishi maisha mazuri. Mshahara wangu ulikuwa mdogo ukilinganisha na kazi nilizofanya. Wazazi wangu walitegemea kwamba ningewaletea pesa ili kuwasaidia na gharama za maisha lakini mimi mwenyewe nilishindwa kujikimu. Sikuwa na raha ingawa nimejifunza kwamba ni muhimu kufanya kazi inayokupa furaha.

**F:** Nimekuelewa. Sasa ukaingiaje kwenye kazi ya uakiolojia?

**M:** Nilikutana na mwanahistoria aliyekuwa mwanaakiolojia ambaye alikuwa akisafiri kwenye meli ambamo nilikuwa nikifanya kazi. Akanihadithia kuhusu anavyochimba mapango na bahari na pia akanipa kitabu cha mwongozo ambacho kiliorodhesha maeneo ambayo mtu anaweza kukuta mengi ya kihistoria. Nilipokisoma nikagundua kwamba ningeweza kuenda kuchimba kwenye sehemu zilizokuwa karibu na mji wangu. Hivyo meli ilipotia nanga niliongozana naye hadi kwangu ambapo tulianza kazi yetu kwa kutembelea sehemu za karibu. Basi ndivyo nilivyoanza kazi mpya.

**F:** Halafu...

**M:** Tulienda kwenye kijiji jirani ambapo kuna magofu mengi sana, yaliyomfurahisha mwanahistoria sana. Sote tulijua kwamba pale tungeweza kuchimba vitu vingi vya kihistoria. Ilibidi kupata kibali kutoka serikalini kabla ya kuanza uchimbaji. Mimi nilishaona filamu kuhusu wachimbaji na nilifikiria kwamba tungepata kila kitu baada ya siku mbili au tatu. Lakini nikagundua kwamba ukweli ni tofauti. Ilibidi kupata vibali na ilibidi kuchimba polepole ili tusiharibu kitu. Tulikaa huko kwa muda wa miezi minne bila kuchoka.

**F:** Kwa hivyo baada ya hapo ukaanza kuchimba mwenyewe?

**M:** Hapana. Ili kuweza kuchimba mwenyewe lazima ufuzu masomo husika. Kwa vile niliacha shule mapema ilibidi niwe msaidizi wa yule mwanahistoria, ambaye alikuwa maarufu katika nchi za Afrika Mashariki. Tulikuwa wasaidizi wengi, tulitoa jasho jingi katika kazi yetu, na tulijifunza mambo mengi sana kila siku. Yeye alitaka sote tujue kila kitu alichokifahamu. Kwa kweli alituona kama warithi wake.

**F:** Inaonekana huyo mwanahistoria alikuwa muhimu sana kwako.

**M:** Bila shaka. Nilikuwa na wasiwasi mwingi kwa ajili ya kutomalizia shule na kukosa cheti, lakini alinipa moyo wa kurudia tena kwenye elimu. Niliamua kusomea kazi hiyo, na licha ya shaka zangu nilifurahia kuongeza ufahamu wa nadharia. Kwa hivyo ingawa nilisoma wakati wa jioni ambapo nilikuwa nimechoka, haikuwa vigumu kwangu.

**F:** Hongera sana, kwa kweli umejitahidi sana.

**M:** Asante. Mara kwa mara huwaza maisha yangekuwaje kama maamuzi yangu yangalikuwa tofauti nilipokuwa kijana. Nina hamu wazazi wangu wangenilazimisha kumaliza shule. Wangalinikataza kuwa baharia na ningalipata mshahara mkubwa zaidi. Kwa kweli ningalikuwa mbali sana hii leo. **

*(Pause 30 seconds.)*

**TLR:** Sasa sikiliza tena.

*(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

**TLR** Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 4, na mwisho wa mtihani.

**Eng:** This is the end of the examination.

© Cambridge University Press & Assessment 2025 

https://xtremepape.rs/

BLANK PAGE

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (Cambridge University Press & Assessment) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

To avoid the issue of disclosure of answer-related information to candidates, all copyright acknowledgements are reproduced online in the Cambridge International Education Copyright Acknowledgements Booklet. This is produced for each series of examinations and is freely available to download at www.cambridgeinternational.org after the live examination series.

Cambridge International Education is the name of our awarding body and a part of Cambridge University Press & Assessment, which is a department of the University of Cambridge.



https://xtremepape.rs/